

Usawiri wa Dini, Mila na Tamaduni za Kiafrika katika Riwaya za Babu Alipofufuka (2001) na Dunia Yao (2006) za Said Ahmed Mohamed na Bina-Adamu! (2002) ya Kyallo Wamitila.

Sylvester Kimugung¹; Dkt. Magdaline Wafula²; Prof. Peter Simatei³.

^{1,2,3}Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu, Chuo Kikuu cha Moi, Kenya.

Main author email: sylvesterkimugung@yahoo.com

IKISIRI

Utafiti huu unanua kuchunguza masuala haya kwa kutumia nadharia ya uhalisiamazingaombwe. Nadharia ya Uhalisiamazingaombwe iliasisiwa na Franz Roh mwaka wa 1925 kama njia ya kukiuka uhalisia na kusawiri dunia ya kisasa iliyotata na ovyo, iliyobutuka, na iliyoparanganyika. Lengo la utafiti ni kuhakiki mitindo ya urejelezi wa dini, mila na tamaduni za Kiafrika na namna inavyowasilisha mivurugo ya jamii katika riwaya teule. Ili kutimiza malengo ya utafiti huu riwaya tatu zimeteuliwa kimaksudi: Babu Alipofufuka (2001) na Dunia Yao (2006) za Said Ahmed Mohamed, na Bina-Adamu! (2002) ya Kyallo Wamitila. Nadharia tete za utafiti ni kuwa riwaya teule zinasawiri mitindo ya uhalisiamazingaombwe ili kuakisi mivurugo ya jamii ya kisasa. Data za utafiti huu umetumia usampuli wa kimaksudi kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Uhalisiamazingaombwe. Utafiti huu ni wa kimaktaba. Riwaya teule na tahakiki mbalimbali zilipatikana maktabani. Data zimechanganuliwa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe na kisha kuwasilishwa kwa njia ya kinathari kwa kutumia madondoo mbalimbali. Utafiti huu ulibaini kuwa matumizi ya dini za Kiafrika zimeonyesha kuwa falsafa za kiafrika zilikuwa zinahakikisha uhusiano mwema baina ya viumbe wote ulimwenguni kuanzia Mungu, mizimu, mizuka, binadamu, vitu vilivyohai na visivyohai. Uhusiano huu ni tofauti na ule wa kimagharibi ambao umekuwa unasisitiza utengano na kusasabisha dunia ya kiulimwengu. Matumizi ya uduara wa wakati umehakikisha watu wameishi kwa usawa, heshima na umoja tofauti na mwelekeo wa kimagharibi wa kistari kimoja ambao ni kandamifu kupitia dhana za ubinafsi na ubepari. Kulikuweco na matumizi ya mila na tamaduni za kiafrika. Mila na tamaduni zilihakikisha kuna maisha mazuri kwa watu wote. Maajilio ya wakoloni yalisambaratisha maisha haya kwa athari hasi kwa malezi ya watoto, mavazi, vyakula na elimu. Utafiti huu ni muhimu kwa kuchangia taaluma kwa kuelewa matumizi ya mitindo ya uhalisiamazingaombwe na namna inavyowasilisha mivurugo ya jamii.

Maneno muhimu: uhalisiamazingaombwe, kusawiri, urejelezi wa dini, mila na tamaduni.

How to cite this article in APA

Kimugung, S., Wafula, M. & Simatei, P. (2021). Usawiri wa Dini, Mila na Tamaduni za Kiafrika katika Riwaya za Babu Alipofufuka (2001) na Dunia Yao (2006) za Said Ahmed Mohamed na Bina-Adamu! (2002) ya Kyallo Wamitila. *Editon Cons. J. Kiswahili*, 3(1), 276-292. <https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v3i1.253>

UTANGULIZI

Karne ya Ishirini na Moja imeshuhudia mivurugo kwa jamii; kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mabadiliko hayo yanatokana na nchi zilizotawaliwa zinapoathiriwa na usasa, utumwa, ukoloni, ukoloni mamboleo, ubepari, utandawazi, na mitalaa ya elimu kutoka nchi zilizoendelea. Inapofanyika hivyo kuna ukandamizaji wa dini, mila na tamaduni za nchi zinazoendelea. Mabadiliko hayo hayawezi kufafanuliwa na uhalisia ambao ulikuwa umezoeleka. Waandishi wa Kiswahili wamebuni mitindo ya uhalisiamazingaombwe ili kuelezea hali hii ya mabadiliko. Lakini matumizi ya mitindo ya uhalisiamazingaombwe umezua kiza zaidi badala ya mwangaza ya hali hii hasa kwa wasomaji.

Mbiti ni mwanateolojia anayejulikana dunia nzima kwa kujenga uhusiano mwema baina ya dini za kimagharibi na dini za kiafrika. Hapo mwanzo kulikuwa na vita vikali baina ya dini za kimagharibi na dini za kiafrika. Kulikuwa na mitazamo potovu kutoka nchi za Kimagharibi kuwa Waafrika wote ni wapagani, washetani, waovu na wasioamini Mungu. Katika kitabu chake *African Religions and Philosophy* (1969), Mbiti alidhihirisha upotovu wa mitazamo hii ya Kimagharibi. Anasema kuwa waafrika ni wanadini kupindukia. Mwaafrika ni mwanadini kabla ya kuzaliwa, akiishi duniani na baada ya kufariki. Mwaafrika anapozaliwa anazaliwa ndani ya dini za Kiafrika. Kila mwaafrika ana dini na hakuna kubadilika (conversion) ili kuingia dini za Kiafrika.

Mila ni taratibu za maisha ya kila siku ya watu, ambayo inahusu sana asili ya watu na hivyo hupokezwa kizazi hadi kizazi. Hivyo, mila hujumuisha mambo kama vile malezi kutoka utotoni hadi uzeeni, miiko, mapokeo, historia, matibabu, matambiko, heshima, adabu na sheria zihusuzo taratibu za jamii kama vile ndoa, uzazi, urithi na vifo. Utamaduni wa watu ni jumla ya matendo, kumbukumbu, matumaini mipango ya mustakabali na hata ndoto zao. Mfumo huu wa kiasili ambao ulijikita katika taratibu za tamaduni maalumu ulivurugwa na

majilio ya wakoloni pamoja na wageni wengine kutoka nchi za Kimagharibi.

Mwenga wa Nadharia

Utafiti huu unaongozwa na nadharia ya uhalisiamazingaombwe ulioanzishwa na Franz Roh (1925) na kuasisiwa na Rettova (2016) na Warnes (2009). Roh katika ufafanuzi wake alikuwa anaegemea upagaji rangi, kwa hivyo utafiti huu umeegemea maoni ya Rettova na Warnes ambao wamefafanua kwa kurejelea fasihi. Kwa mujibu wa Rettova (2016) nadharia ya uhalisiamazingaombwe umechipuka wakati ambapo dini, mila na tamaduni za kiafrika zinavyopingwa na falsafa za Kimagharibi. Falsafa hizi za kimagharibi ni sayansi, urazini na uhalisia. Wamagharibi wanaamini itikadi hizi na walitenga chochote ambacho hakikuwa kinahusiana nacho. Mitazamo hii imefanya watafiti wa Kimagharibi kuamini sayansi, urazini na uhalisia kama njia pekee ya kupata maarifa. Mitazamo hii imeenezwa kama simulizi kuu kote duniani. Wamepuuza mitazamo mingine ya kuelewa dunia kutoka jamii zingine. Ikumbukwe kwamba simulizi kuu zinapokuwa kama njia pekee ya kuhodhi ukweli, mwishowe zinaporomoka. Zinaporomoka na kuunda simulizi ndogo ndogo zinazoeleweka na jamii mahususi katika miktadha yao. Simulizi ndogo ndogo ya imani inakataa matumizi ya simulizi kuu ya sayansi na urazini; inapendekeza matumizi ya maarifa ya jamii mahususi (indigenous thought systems). Kuchipua maarifa ya jamii ya dini, mila na tamaduni za Waafrika.

Warnes (2009) anasisitiza mwelekeo unaoitwa nadharia ya imani ya uhalisiamazingaombwe (faith base magical realism). Imani katika muktadha huu ni ukweli ambao huwezi kuthibitishwa kisayansi au kirazini. Ni Imani hii ndio inamfanya msomaji kuacha urazini na usayansi na kuwa na fikra pevu kuhusu matukio duniani (expanded sense of reality), hivyo basi kuamini dini, mila na tamaduni za jamii yake. Katika sehemu ifuatayo tumeanza kwa kujadili dini na kisha mila na tamaduni za kiafrika.

Dini za Kiafrika

Dini ni mchakato mzima wa maisha ya jamii. Binadamu anapofikiria kuhusu dini anaanza na dunia ya kifikirivu isiyohalisi. Hivyo kuzua dunia ambayo si halisia. Hii inapiku kaida za kisayansi za kimagharibi. Waandsihi wa riwaya zinazoangazia dini za kiafrika wanatumia mitindo ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe kusawiri maswala ya dini kama inavyojitokeza katika riwaya teule za utafiti (Warnes 2009, Rodney 2015).

Dini za Kiafrika zinafalsafa tofauti ukilinganisha na falsafa zinazotokana na dini za Kimagharibi. Mojawapo wa falsafa hizi ni utengano wa dini na maisha ya kidunia (secular world). Dini za kimagharibi zimetenganisha dini na maisha ya dunia. Wao wanasema kuwa dini ina mahala pake tofauti na mambo ya dunia ambayo yana matukio yake tofauti. Kuzua dhana ya maisha ya kiulimwengu (secularization). Ni maisha ya kiulimwengu yaliyopulizia moto itikadi za kibepari duniani kote. Dini za kiafrika hazina utengano huu, dini na maisha ya kidunia ni mambo moja. Nchi za Kimagharibi zina mtazamo wa uwepo wa binadamu ilhali dini za Kiafrika zinaamini nguvu fulani ambayo ina msugumo wa uhai wa binadamu. Msugumo huu unatokana na Mungu, mizimu (Spirits), mizuka (ancestors) (Mbiti, 1969). Katika sehemu hii utafiti umehakiki dini za kiafrika.

Mipangilio ya Viumbe Duniani na Uduara wa Wakati katika Dini za Kiafrika

Wafrika wanaelewa kuwa viumbe ulimwenguni wamegawika katika sehemu mbili; sehemu inayoonekana (Dunia) na sehemu isiyonekana (Anga). Anga ndiyo sehemu inayoaminiwa kuwa Mungu ndiye anaishi. Kwa mujibu wa (Mbiti, 1969) ulimwengu huu umewekwa katika migawiko saba kama ivyodhihirika:

1. Upeo wa juu kuna Mungu (God). Inaaminika kuwa Mungu aliumba kila kitu kilichoko duniani na Yeye ndiye uhai.
2. Sehemu ya pili ni Umungu (Divinities). Hii ni sehemu inayowakilisha kazi za Mungu aliyekatika upeo wa juu. Kazi za Mungu zinadhihirika kupitia sehemu hii ya Umungu.
3. Sehemu ya tatu ni mizimu (Spirits). Mizimu ni watu waliofariki kitambo sana na wamesahaulika na waliohai duniani.
4. Sehemu ya nne ni mizuka (Ancestors). Mizuka ni watu waliofariki majuzi. Bado wanakumbukwa na waliohai kwa majina.
5. Sehemu ya tano ni binadamu walio hai na wale ambao watazaliwa.
6. Sehemu ya sita ni viumbe waliohai kama wanyama, na mimea. Viumbe hawa wanatumia na wanadamu kama vyakula.
7. Sehemu ya saba ni vitu visivyohai kama mawe, mvua, mito n.k.

Orodha hii ndio msingi mkuu wa dini za Kiafrika. Viumbe vyote vilikuwa vinahusiana kuanzia upeo wa juu (Mungu) hadi chini (vitu visivyohai). Kila sehemu ilikuwa na uhusiano kuanzia sehemu ya juu hadi chini. Dini za Kiafrika zinaakikisha kuwa wafrika wanapata nguvu kutokana kwa Mungu, mizimu na mizuka na uhusiano mzuri kutoka kwa wanyama, mimea, miti, ili wafrika waweze kuishi vizuri kiafya, kimali na kimaisha. Dhana ya uhusiano baina ya viumbe ulisambaratika wakati ambapo kulikuwa na maajilio ya wakoloni na dini ya Kikristo. Katika mtazamo wa dini za Kimagharibi, hakuna uhusiano wowote kati ya viumbe hawa. Kuna utengano mkubwa sana. Simulizi kuu za nchi za Kimagharibi zilipoenezwa duniani, ilionekana kuwa dini/imani za Kiafrika hazina maana na hivyo zinapaswa kukiukwa. Wakoloni waliona kuwa wafrika hawana dini na kuwa wanafaa kubadilishwa (converted). Kwa mujibu wa Mbiti (1969) wakati katika mtazamo wa Wafrika ulikuwa wa haina mbili tu. Wakati uliopita

(zamani) na wakati uliopo (sasa). Waafrika hawakuwa na dhana ya wakati ujao. Wakati ujao ulikuwa lazima ni dhahirishi na kuwa ni vitendo vinyoweza kutendwa tu. Mtazamo huu uliwasaidia Waafrika kuishi pamoja bila kunyanyasana au kukandamizana. Hii ni tofauti na wakati wa kistari kimoja. Wakati wa kistari kimoja ulitokana na mtazamo wa kimagharibi. Mtazamo huu unahusu wakati kuwa na mwanzo na mwisho; jana, leo na kesho. Ni dhana hii ya wakati wa mstari ndiyo inafanya watu kuwa wanyanyasaji, fisadi na wadhulumu. Hii inabainika katika riwaya ya BAF, K anapoishi jijini anakuwa mfungwa wa wakati wa kistari kimoja na hivyo basi kuwa fisadi na mbinafsi.

Nasema nanyi mahakimuwakati ... Nyinyi mso mwanzo wala mwisho. Nyinyi wa zamani na wa sasa. Mpo katika kutokuwepo. Manaokufa huku mkiishi. Nyinyi mnaoona yote. Mnaosikia yote. Msoweza kukimbilika. Wenye kupiga na kuharibu na kupanga na kutengeneza wakati moja. Nyinyi sehemu ya mimi, ninakuja. (BAF, 41)

Wakati katika dini za kiafrika si muhimu. Kilicho muhimu ni utekelezaji wa kitendo. Kwa mfano kila mwaka una matendo mbalimbali ambayo lazima yatimilizike. Kuna uwezekano mwaka ukawa si sawa. Hivyo basi tarehe na kalenda katika dini za kiafrika sio muhimu. Kiafrika hakuna kalenda. Katika dini za kiafrika hakuna mwisho wa wakati. Hakuna mwisho wa dunia. Hakuna kile ambacho wakristo wanaita dunia ya pili au mbinguni. Maisha yalikuwa kwenye mwingo. Kuzaliwa, kukua, kufariki na kuzaliwa kiupya. Mzuka anamwambia K:

Nimefufuka kitambo...au tuseme roho zimo katika duru ya wakati wa daima usiomalizika. Ndiyo kusema hatukufa. Hatufi, wala hatutakufa. Hupotea kwenye macho yenu tu. (BAF, 20)

Nukuu hii ya BAF inatujaza kuwa Imani za Kiafrika ni tofauti za Kimagharibi. Mtu anazaliwa, kukua na anapofariki hakuna mbinguni ya Kikristo. Yaani kiafrika mtu anapofariki huwa anapotea tu machoni mwa waliohai. Anaendelea kuishi nao kiupya. Katika muktadha huu kama Mzuka wa riwaya ya BAF. Dini za Kimagharibi ziligeuka dhana ya uduara wa wakati na kusababisha mstari wa laini. Ni ukiushi huu ndio utafiti huu ulibaini kuwa ndio kukawa chanzo cha changamoto zinazokumba jamii:

Ukiushi wa Dini za Kiafrika na Mivurugo ya Jamii ya Leo

Katika sehemu hii mtafiti amejadili jinsi dini/imani za Kiafrika zilivyokuwa na falsafa ya utu, upendo na uhusiano kwa viumbe vyote duniani. Ijapokuwa kutokana na kuzuka kwa falsafa za Kimagharibi; Waafrika waliacha dini/imani za Kiafrika na kubukia falsafa za Kimagharibi na hivyo basi kusababisha mivurugo ya jamii inayoshuhudiwa sasa. Falsafa hizo ziliuhusisha utengano wa viumbe duniani na hivyo basi kusababisha ubinafsi miongoni mwa binadamu, uchafuzi wa mazingira na kuzuka kwa jamii ya leo iliyotata na ovyo, iliyobutuka, iliyoparanganyika, inayotuchezesha foliti za mauti, inayonata utamu wa kifo na uchungu wa uhai. Waandishi wa riwaya za uhalisiamazingaombwe wanaonyesha kuwa mivurugo ya jamii imetokana na Waafrika kukaidi uhasilia wao. Hivyo basi riwaya zao kuwa na maegemeo ya maudhui ya dini, mila, na tamaduni za kiafrika. Maegemeo hayo yanaoana na maoni ya Warnes kuhusu riwaya za Uhalisiamazingaombwe:

Iwapo matini itakuwa na maegemeo katika tamaduni fulani iliyo tofauti na tamaduni za Kimagharibi, basi riwaya hizo zitatumia mitindo ya nadharia ya uhalisiamazingaombwe. Nadharia hii itamwezesha mwandishi kutumia dini, mila na tamaduni za jamii husika. (Warnes 2009: 15)

Katika sehemu ifuatayo utafiti huu utaelezea maegemeo hayo ya dini, mila na utamaduni za Kiafrika na kutokana

na ukiushi wao ulivyosababisha mivurugo ya jamii ya kisasa.

Uhusiano kati ya Binadamu na Mungu

Kwa mujibu wa Mbiti (1989) ‘popote alipo mwafrika, dini yake ipo hapo’ msemu huu wa Mbiti unamaanisha kuwa hakuna tofauti kati ya maisha ya mwafrika na dini yake au Mungu wake. Kwa maneno mengine hakuna kutenganisha Mwafrika na dini yake. Mathalan, Mwafrika anapofanya kazi yake yu pamoja na dini yake. Katika riwaya ya BAF, imani/dini za Kiafrika zinawakilishwa na mhusika Mzuka:

Wakati ule wa akina Gwari, uleo-wa-mawazo ya kigeni tayari ulikuwa umeshaganda vichwani mwa watu wetu. Mimi nasimulia kale ya kale kabla ya hapo! (BAF, 1)

Wakati huu watu walikuwa wanaamini dini za Kiafrika na mitazamo yake. Mitazamo hii ilikiukwa katika ujio wa dini ya Kikristo katika mtazamo wa Kimagharibi. Katika mtazamo wa Kimagharibi Dini na Binadamu ni vitu viwili tofauti; kuna utengano:

Kuna pingamizi bila shaka. K haamini [...], ela ule wa Yesu. Sijui kwa nini amekuwa hivi siku hizi! Zamani sote tuliamni. (BAF, 1)

Utengano huu wa maisha halisia na dini katika dini ya Kikristo inawakilishwa na mhusika K. K na Mzuka ni wahusika mwenye falsafa tofauti maishani. Mzuka kutokana na falsafa ya dini za Kiafrika ni mhusika ambaye anajali maslahi ya wengine maishani mwake, anapomwona K akiishi maisha ya raha na raia wake wanateseka katika lindi la umaskini, anamtafuta ili amwambie mateso ya watu wake (BAF, 1).

K ni mhusika anayetokana na falsafa ya utengano kati ya dini na maisha halisia. Kama inavyojitokeza katika riwaya, K ni mhusika dhalimu kupindukia kutokana na falsafa hii:

Kila mtu anafwata shengeshwa akiongozwa na hamasa na hisia, na hatimaye kukubali kukaliwa juu na watu waovu... watu wenye kulimbikiza

utashi wao katika vinganja vyao vidogo. (BAF, 148)

Ni falsafa hii ya utengano ndio inamfanya K kuwadharau watu. K alikuwa anaafadhalisha watu walale njaa lakini mbwa wake ale na ashibe. Dunia yake inasawiriwa na gari la kifahari *limonsin*, kasri kama Dracula, kilabu cha *Neo-Casino*, matumizi ya dawa za kulevya, ukahaba, unyang’anyi wa wake wa watu na uvaaji wa miwani ili raia wake wasimwone. Dhihirisho ya uovu unaendelezwa na falsafa ya utengano wa Kimagharibi. Kwa mujibu wa (Mbiti, 1969) dini za kiafrika zinahusisha mtu kutenda wema saa zote. Hii ni kwa sababu yu pamoja na dini yake. Lakini falsafa ya kimagharibi mtu ametengwa na dini yake. Wakati ambapo hayuko na dini yake (dini ya kimagharibi) anaanza kutenda maovu. Mzuka anamkataza K kuwa maisha hiyo si sawa. Wakati wake, mbwa alikuwa akikula baada ya watu wote wa ukoo kukula na kushiba (BAF, 2).

Uhusiano wa Binadamu na Wanyama

Waafrika wanaamini kuwa wanyama waliumbwa pamoja na binadamu. Kwa mfano Maasai wanaamini kuwa walipewa ng’ombe na Mungu na hakuna kabila lingine linaloweza kumiliki. Hii ilikuwa imewafanya wakiona kabila lingine wananyag’ua bila kufikiria kuwa wanaiba. Waafrika wanaona wanyama kama ishara ya uwepo wa Mungu, miungu na roho. Hivyo basi wanatunzwa vizuri (Murdock, 1959). Katika riwaya ya BA, kuna uhusiano wa karibu kati ya ndege na Mungu katika nchi ya Zakongwe:

Nilipozindikana nilikuwa nimezungukwa na watu wengi ajabu: wanawake kwa wanaume. Nyuma huko niliweza kuwasikia watoto waliokuwa wakiigizwa sauti za ndege na wanyama. Niliyafungua macho yangu polepole na kuangalia huku na kule. Pua yangu iliweza kuinusa hewa iliyochanganyikana na harufu ya nyama iliyokuwa ikiokwa. (BA, 16)

Uiigizaji wa sauti ya ndege inadhihirsha jinsi watu walikuwa wakiabudu Mungu katika dini za Kiafrika. Mojawapo ya njia za kuabudu ni kutoa kafara. Waafrika walikuwa wanatoa kafara ya wanyama kama ndege, ng'ombe, mbuzi na kondoo. Hii ndiyo harufu ya nyama iliokuwa ikiokwa katika dondoo hili. Rangi ya wanyama hawa ilikuwa inafaa kuwa moja kama nyeusi au nyeupe. Kafara hii ilikuwa kama njia ya kushukuru Mungu kwa uhai au mavuno, kumtambua Mungu kuwa mmiliki wa wanyama hawa, kuomba baraka kama mvua na kuondoa mabaya yasiitukie maishani mwao (Mbiti, 1969).

Katika Dini za Kiafrika madaktari wa kienyeji (medicinemen) wanapatikana katika jamii. Madaktari hawa wanajulikana kwa uponyaji wa magonjwa mbalimbali katika jamii. Wakoloni waliona madaktari hao kama watu waovu katika jamii. Waliwaita warogi. Hata hivyo madaktari wa kienyeji walikuwa wanatekeleza majukumu mbalimbali katika jamii kama inavyojitokeza katika riwaya ya BA:

Nilipoelekea huko niliona mijusi waliokuwa wakiota jua wakikimbilia usalama sehemu ya chini. Nilitembea polepole hadi nilipofika hapo na kuuweka mfuko wangu juu ya jabali hilo. Hapa na pale palikuwa na alama za vinyesi vya mijusi. Niliviangalia vile vyeupe. Nakumbuka zamani walivitumia vijana kijijini kujipaka tine zao baada ya kutahiriwa na ilisemwa kuwa viliharakisha uponaji au wakati mwingine kutibiwa na madaktari wa kienyeji. (BA, 80)

Madaktari wa kienyeji walikuwa na kazi muhimu ya kutibu wagonjwa katika jamii zao. Walikuwa wanatumia aina mbalimbali za dawa za mimea na sehemu za wanyama, utoaji wa kafara, sherehe za mivigha ili kutoa ugonjwa. Katika dondoo hili, vinyesi vya mijusi vinatumia kupona tine za watahiriwa. Aidha, iwapo ugonjwa si wa hali ya juu mtu anaweza kujitibu kwa kujitafutia dawa mwenyewe kutoka mimea.

Mila na Tamaduni za Waafrika zilikuwa zinahusisha heshima kwa wanyama. Kinaya ni kuwa K, katika riwaya ya BAF, anachora Kasri lake kwa mchoro wa mnyama anayeitwa guruguru:

Mchoro aliochorewa na rafiki yake mwenye sura ya guruguru anayeitwa *Baseball*, kwa nuio zake mwenyewe alivyotaka uonekane. (BAF, 15)

Guruguru ni mjusi mkubwa ambaye anapenda kuishi chini ya ardhi. K kuchora nyumba yake kama guruguru ni jazanda ya uchukivu wa K kwa dini za Kiafrika. Guruguru ni mnyama ambaye katika mila na tamaduni za Kiafrika anafaa kuchungwa na kutolewa kafara. Ikumbukwe kuwa alikuwa haamini tena katika dini za Kiafrika. Kwa hivyo K kuchora nyumba yake kwa sura ya guruguru ni sawia na matumizi mabaya ya dini za kiafrika.

Dini za Kiafrika zilikuwa na mtabiri. Hawa ni watu ambao wana nguvu maalumu ya kutabiri yajayo. Wanapata nguvu hizo kupitia ndoto. Wanaonya jamii kuhusu masuala mbalimbali. Haya yanaonekana katika riwaya ya BA:

Siku moja jioni watakuja watu watakaokuwa wametia moto mifukoni. Naona pia nyoka mrefu atakayenyiririka kutoka Kisiwani hadi ziwa la Sango. Atakuwa wa ajabu nyoka; watu watakuwa wakitokea tumboni! (BA, 18)

Nyoka katika dondoo hili linaashiria utabiri wa mtabiri katika dini za kiafrika. Utabiri huu ulikuwa ni ujio wa wakoloni katika nchi ya Kenya na ujenzi wa reli. Ulitimia wakati ambapo *British* ilitawala Kenya mwaka wa 1885 hadi 1960.

Uhusiano kati ya Binadamu na Mimea (plants) na Vitu-visivyohai (non-living things)

Tangu kale Waafrika wamekuwa na maadili mema ya kutunza mazingira. Maadili haya yalitokana na mtazamo chanya ya ontolojia, cosmolojia, utabibu na uponyaji. Aidha, mazingira kwa waafrika ni takatifu na yanahusiana

na viumbe wengine duniani na hivyo yanafaa kutunzwa. Waafrika wanaona mimea kama usawiri wa uwepo wa Mungu, miungu na roho. Hivyo basi inafaa kutumiwa vizuri bila kuharibiwa. Mbiti anasisitiza hoja hii anaposema mawe sio vitu bure, ni mawe ya dini (Mbiti 1969, Murdock, 1959). Ni kutokana na falsafa hii ya dini za Kiafrika iliyowapelekea waafrika kutunza mazingira yao. Haya yalibadilika kwa maajilio ya dini za kimagharibi iliyosisitiza utengano wa dini na mazingira. Hii imepelekea mazingira kuharibiwa kama inavyobainika katika riwaya ya BA:

Basi umetufaa hata sisi lakini wanasema huenda maji yake yakakaushwa na jua hili au hata huenda hali ya hewa ikaharibika kisha barafu ikayazizima maji na kuyageuza theluji tupu! (BA, 43)

Dondoo hili linatusawiria uharibifu wa ozoni-leya. Ozoni-leya ni ukanda unaozuia miale ya jua isiwafikie binadamu na kuwadhuru. Tafiti zilizofanywa na wanasayansi zinaonyesha kuwa ukanda huu umeharibiwa na kemikali za CFCs. Uharibifu huu umesababisha miale ya jua kuongezeka duniani na kusababisha saratani ya ngozi, uhai wa majini na ardhini kuwa mgumu. Aidha, barafu kunyenyuka na maji kuongezeka kwenye miambao ya pwani (Kegley na Raymond, 2014).

Murdock (1959) anasema kuwa waafrika hawana dhana ya vitu-visivyohai. Kila kitu kina uhai wa aina fulani. Kwa mfano mawe ina nguvu ndani mwake. Nguvu hii ndiyo inayotumiwa na wahubiri, viongozi, na wajenzi kutimizia kazi zao. Hakuna utengano wa aina yoyote. Dhana ya utengano wa vitu-visivyohai na viumbe wengine katika dunia inaendelezwa na nchi za Kimagharibi. Katika tamaduni za Kiafrika, miti zinahusisha uhai. Haya yanabainika katika riwaya ya DY, pale Mize anaposhika mmea kwa kidole na inakua (DY, 64). Hii inaonyesha kuwa binadamu anafaa kujukumika kuhakikisha kuwa ametunza mazingira yake ikiwemo miti.

Mwandishi Wamitila ametumia simulizi za jadi katika kazi yake kuwa jamii lazima iheshimu viumbe wote duniani:

Mwanaume atakayeenda huko anaweza kushtukia amebadilika jinsia na kuwa mwanamke kwa kuwa lazima alizunguke jabali kubwa lililoko hapo. Haya ndiyo matokeo yake. (BA,9)

Mwandishi huyu ametumia kisasili hiki kuonyesha umuhimu wa kutunza mazingira katika jamii za Kiafrika. Yeyote ambaye ataliheshimu jabali hilo. Jabali lina nguvu fulani ambayo inaweza kuathiri mtu maishani mwake. Hivyo basi mazingira yanafaa kutunzwa vilivyo.

Katika kazi za kihalisiajabu mazingira huwa sehemu muhimu sana. Aidha, mimea, mito mikubwa na bahari huchukua sehemu muhimu katika kazi hizi. K anapokuwa akipeleka na mzuka nyumbani kwao alikozaliwa, (baada yao kugeuka na kuwa mchwa), wanatumikia ardhini kupitia chini kwenye mizizi ya gugu la ukoka (BAF, 84). Aidha, K anapokuwa akirudi kwake kutoka kwao, mwandishi anatumia kwamba anafyokonyoka kutoka kitundu kidogo chanjia ya mchwa kutoka chini ya ardhi (BAF, 145).

Babu yake K anapomaliza kazi yake anayosema alikuwa ametumia kufanya kumhusu K, anarudi kwa wafu kupitia baharini. Aidha, mahakimuwakati wanaishi baharini na huku ndiko wanakomhukumia K. Baada ya kumlisha kiapo wanamrusa majini na wao pia wanarudi kuko huko majini. Mahakimuwakati wanapokuwa wakitambika na kutengeneza Kithitu cha Kikamba, wanatumia mchanganyiko wa vitu vingi. Vitu kama vile meno ya fisi, karafuu na karafuu maiti (haya ni manukato fulani anayotiwa maiti wa Kiislamu wakati wa kupambwa kabla ya kuzikwa), mizizi ya mimea ya kaburini, unyoya wa juu wa korongo wa Uganda na magamba ya samaki ya tilapia kutoka Ziwa Nyasa na Ziwa Rudolf la Kenya, Ziwa la Tanganyika na Nduaro. Aidha, walitumia majani ya miti minyiriro na mwarubaini (BAF, 144). Mazingira haya ni

muhimu sana kwa sababu wahusika wa uhalisiajabu huvunja mipaka ya kimasafa. Mimitu, bahari na mito ni vyombo vya kupitiwa na hawa wahusika wanapohusika katika kazi ya fasihi. Ili kufanikisha kazi yake ya kihalisiajabu, mwandishi hana budi kutumia mazingira kwa kuwasilishia ujumbe wake.

Uhusiano wa Binadamu na Mizuka (ancestors)

Katika mipangilio ya viumbe duniani, mizuka inapatikana katika sehemu ya nne. Mizuka ni binadamu ambao walifariki kitambo lakini bado jamii wanawakumbuka. Mara nyingi ni mwanzilishi wa ukoo. Jina lake bado linakumbukwa na wanajamii. Katika riwaya ya BAF sehemu hii inawakilishwa na Mzuka. Kwa mujibu wa Murdock (1959) mizuka inajulikana kwa vizazi vitano kabla haijasahaulika na waliohai. Hii ni kwa sababu mchakato mzima wa kufariki hujamalizika. Yaani kwa pamoja wafu hai- si wafu si hai. Wako katikati. Mguu moja uko kwa uwafu na mguu mwingine uko kwa uhai. Wafu hai watasahaulika baada ya kizazi chake kifariki chote. Mzuka ni wafu hai. Hii ni kwa sababu bado anajulikana na waliohai.

Maajuzi anatuambia alikuwa babu yake.

Mizuka wanaweza kuzaliwa upya katika jamii. Mtoto anayezaliwa upya huwa si lazima wafanane na mizuka hiyo shilingi kwa ya pili. Mara nyingi baadhi ya sifa zake zitajitokeza kama masikio au kichwa. Mtoto huyu anapewa jina la mzuka huyo. Katika riwaya ya DY, Kilua ni kama mzuka. Kilua alizaliwa upya kwa umbo na sura ya Bisudi. Katika sehemu ifuatayo mtafiti ameangalia majukumu ya mizuka hawa na kuonyesha kuwa jamii ya leo imevurugika kwa sababu haitambui majukumu yao tena.

Mizuka walikuwa wanaheshimiwa na waliohai. Waliohai walikuwa wakiadhimisha tambiko/sadaka ya kinywaji (mvinyo, maziwa n.k.) kama inavyojitokeza katika riwaya ya DY:

Sasa lilikwenda tena kwenye kivuli cha meza, likainua kile kibuyu cha kilewevu, likainua pembe ya urithi ya faru na kuijaza kilewevu. Likawa linapita likimwaya matone ya kilewevu huku likisema. Hii ya Lumumba, hii ya Neto, hii ya Cabrel, hii ya Rodeny, hii ya Samora... Na...na...na... Orodha ya waliopewa kinywaji pasi na kuonekana ilikuwa ndefu. (DY, 193)

Mwandishi anatueleza jinsi waafrika walikuwa wakifanya matambiko hayo kabla ya kuja kwa wakoloni na falsafa zao za Kikristo. Hii ni kwa sababu waafrika waliona umuhimu wa mizuka maishani mwao. Matambiko hayo yalifanywa kutegemea kabila. Makabila mengine yalikuwa yakifanya kila wakati na mengine mara chache. Wakati wa matambiko kuna kutaja majina yao, kama walivyokuwa wakiitwa wakiwa hai. Matambiko hayo yanafanyika katika sherehe mbalimbali kama siku ya tohara, uzaaji na utoaji majina ya watoto na wakati wa maombi ya kila siku. Ni vizuri kujua kuwa mizuka walifariki wakiwa na umri mkubwa. Waliokufa wakiwa watoto, wasiooa na waovu hawawezi kuwa mizuka katika dini za kiafrika (Mbiti, 1969).

Sehemu za makaburi ya mizuka zilikuwa zinahifadhiwa katika jamii, kulikuwa na miko. Lakini jamii ya leo hawana miko tena. Hii inabainika katika riwaya ya BA, Binadamu alipokuwa Marekani alipata watu wakifufua mwili wa Albert Einstein:

Kwa nini Albert Einstein alikuwa na akili ya ajabu. Tunachunguza ubongo wake sasa! Ubongo wake? Tuliufukua baada ya kifo chake! Huku hamna miko? Baada ya kifo aliipoteza haki ya mwili wake. Tunachunguza kiini ili kuiendeleza jamii ya kesho. (BA, 128)

Dini za kiafrika zilikuwa zinahifadhi makaburi ya mizuka kwa sababu yaliadiniwa kuwa makao yao. Mizuka walikuwa wanaishi sehemu hiyo na kuharibu ilikuwa

sawia na kuikosea heshima. Hii inadhihirisha jinsi watu wamekengeuka kutokana na utamaduni wa Kimagharibi. Ni kutokana na kukaidi dini za Kiafrika ndipo mivurugo ya jamii ikaenea katika jamii ya leo. Riwaya ya BAF, imeonyesha jinsi mizuka walivyohai kwa mujibu wa mila na tamaduni za Kiafrika:

Kwamba hatupotei tunapita tu, kutoka ng'ambo moja kwenda nyengine, dunia ya kuwepo katika ombwe na ububu. Katika kukamilisha duara...labda hivyo [...]. Simulizi za zamani zinasema kuwa roho zinapokwisha toka ndani ya miili ya watu hugeuka vivuli vinavyoishi. (BAF, 1:119)

Hii ni dhihirisho tosha kuwa mizuka wanaishi japo wamefariki kitambo. Hivyo basi walikuwa na majukumu yafuatayo:

Mizuka wanawapa ushauri watu wa ukoo yake kuhusiana na changamoto mbalimbali wanazokumbana nayo. Hii inabainika katika riwaya ya BAF, kupitia mhusika Mzuka. Mzuka alikuwa mwanzilishi wa ukoo wa Amani. Hata hivyo alipoona watu wa ukoo wake wanateseka alikuja duniani ili atatue changamoto hizo. Mzuka alibaini kuwa changamoto zinazokumba koo zake zinatokana na kiongozi K. K alikuwa amechaguliwa ili kuwasaidia watu lakini aliwatelekeza na kwenda kuishi mijini. Ilikuwa vigumu raia wake kumfikia kwa sababu alikuwa mbali na hao. Mzuka alikuja moja kwa moja ili amshauri jinsi anafaa kufanya ili ukoo wake waishi namna walivyokuwa wakiishi yeye akiwa hai. Japo K alikataa hapo awali kutokana na maingiliano yake na tamaduni za Kimagharibi na kusema kuwa yeye hamini tena ufufuzi wa miili, (BAF, 1) mwishowe alishaurika; baada ya Mzuka kumpeleka nyumbani na kumuonyesha jinsi watu wanavyoteseka.

Mizuka wanalinda dini, mila na tamaduni ya ukoo na jamii kwa ujumla. Mzuka alipoona kuwa watu wa jamii yake wanakaidi mila na utamaduni alikuja kuwaelekeza. Utamaduni wa jamii ulikuwa umepotea kupitia mhusika K

ambaye alikuwa ameiga tamaduni za kigeni. Tamaduni hizo zilikuwa hasi. Baadhi yao ni kuunda vilabu vya burudani kama **Neo-Casino** na FKK ambapo watu walikuwa wanaenda wakiwa uchi, kujishirikisha kwenye ukahaba, ushoga na matumizi ya dawa za kulevya. K alikuwa na hulka za ubinafsi, ujenzi wa nyumba za kifahari ilhali raia hawana nyumba, kulisha doggy ilhali raia hawana vyakula. Ilibidi Mzuka aje moja kwa moja kumwambia K kuwa hizo zi tamaduni zao. Tamaduni zao zilikuwa zinahusisha upendo, utu, umoja na ushirikiano baina ya binadamu ili kuendeleza jamii.

Kuwaonya waliohai kwa tabia zisizofaa na kuwaadhibu. Jamii ya K ilikuwa na tabia zisizofaa katika jamii. Hii ilipelekea Mzuka kukujia K kwa njia ya ndoto ili kumwonya. Inavyobainika katika riwaya, tabia za kimagharibi zilikuwa zimevingia K hadi ikawa vigumu kuacha tamaduni hizo ngeni. Ilibidi Mzuka kumwadhibu na kumhukumu K. K alikataa kwenda kijijini kuwaona raia wake ambao walikuwa wamemchagua. Njia pekee iliyomweza K ni Mzuka kumlazimisha kuvaa figu ili afike kijijini mwake. Safari hiyo ilikuwa ngumu kwa K. Safarini kulikuwa na joto sana lakini ilibidi K avumilie. Kuvumilia ilikuwa kama njia moja ya kumwadhibu K ili ajue kuwa watu wanaangamia. Anapokuwa katika kijiji chake, nguo zake zinaibiwa. Zaidi ya hayo alishuhudia moja kwa moja jinsi watu wanavyoteseka hadi wengine wanajitia kitanzi kama Kali. Zaidi ya hayo, kwa sababu ya ukosefu wa chakula watu wanakula matunda inayotundwa kutoka msituni. Aidha, K anapitia magari ya umma ambayo yalikuwa yanaharibika njiani kila mara.

Upeo wa adhabu yake ni kuhukumumiwa na mahakimu wakati na kutiwa majini. Mwishowe anafariki kifo cha chungu:

Umeshtakiwa na roho nyingi ulizokatisha tamaa au hata kuziangamiza kabisakabisa kwa ulaghai na uhasidi wako. (BAF, 73)

K alikuwa amekatisha roho nyingi kutokana na uongozi wake mbaya na ilibidi tu aangamizwe. Mzuka pekee ndiye alimweza kumwadhibu.

Mila na Tamaduni za Waafrika na Mivurugo ya Jamii

Kyamba (2018) akimrejelea Madumulla (1988) anasema kuwa mila ni taratibu za maisha ya kila siku ya watu, ambayo inahusu sana asili ya watu na hivyo hupokezwa kizazi hadi kizazi. Hivyo, mila hujumuisha mambo kama vile malezi kutoka utotoni hadi uzeeni, miiko, mapokeo, historia, matibabu, matambiko, heshima, adabu na sheria zihusuzo taratibu za jamii kama vile ndoa, uzazi, urithi na vifo. Kwa vile mila hizi ni tunu kwa jamii husika, jamii hiyo huwa tayari kuzitetea kwa hali yoyote ile. Mila kwa namna fulani ni katiba ya jamii ambayo hutokana na uzoefu wa watu wenyewe. Ni katiba hii ndio iliyowezesha jamii iishi kwa amani, upendo na ushirikiano. Kwa upande mwingine utamaduni ni namna ya maisha na jinsi watu wa jamii mahususi kwenye kipindi maalum katika historia huku wakiitikia changamoto za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Hakika utamaduni wa watu ni jumla ya matendo, kumbukumbu, matumaini mipango ya mustakabali na hata ndoto zao (Mwita- ssemenda, 2005). Aidha, Ndungo (1992) anasema kuwa utamaduni unahusu mila, asili, jadi, na desturi za mavazi, vyakula, imani, tabia, na maisha ya jamii kwa ujumla. Kwa maoni yangu mila na utamaduni ni jumla ya maisha ambayo mtu anaishi. Maisha hayo ni kuwa na heshima kwa watu wote kuanzia wadogo mpaka wakubwa. Chochote utendacho lazima ungalie mwingine. Maisha hayo ni kwa manufaa kwa watu wote katika jamii. Mila ni matendo kwa ujumla ya binadamu katika miktadha maalum. Matendo hayo yanakubalika kijamii na haina athari hasi kwa maisha ya binadamu.

Mfumo huu wa kiasili ambao ulijikita katika taratibu za tamaduni maalumu ulivurugwa na majilio ya wakoloni pamoja na wageni wengine kutoka nchi za Kimagharibi.

Mtagusano na wageni hawa ulivuruga utaratibu wa mifumo ya maisha ambayo yalikuwako. Mazrui anasema: Bara la Uropa lilikuwa tayari kutuachia (bara la Afrika) dini, lugha na tamaduni zao kwa kubadilisha na mashamba, madini, nguvukazi na vitu vingine vya kiuchumi vilivyo barani mwetu. (Mazrui 1993:6)

Hii ilipelekea kuporomoka kwa maadili ya jamii. Waafrika walipigania mila ya watu wengine wasiojua asili yao wala umuhimu wao. Ikumbukwe kwamba mila inapohamishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine, wanaoiga mila hiyo watakuwa kama watumwa. La kushangaza zaidi ni kuwa wakoloni hawa walichukua mali ya Afrika ambayo yangetumika katika maendeleo. Matokeo ni waafrika walipoteza mila na mali yao!

Kwa mujibu Paul na Robin (2007) katika K21 utandawazi umefanya tamaduni kutoka jamii zingine (hasa za kimagharibi) kuingilia tamaduni za jamii nyingine (hasa za bara la Afrika). Mwingiliano huu wa utamaduni umekuwa na athari zifuatazo:

1. Tamaduni za jamii mbalimbali zimesambazwa katika jamii nyingine na jamii husika kuiga tamaduni hizo na hata kufanya kuwa tamaduni zao.
2. Kupitia mitandao ya kijamii, televisheni, na filamu; picha mbalimbali za tamaduni ngeni zinaweza kusambazwa duniani kote na wenyeji kuweza kufasiri maana ya ishara mbalimbali za tamaduni hizo ngeni.
3. Dunia imekuwa kijiji hasa kutokana na matumizi ya teknolojia na usafiri wa kisasa. Hii imewezekana, kwa mfano utazamaji wa michezo ya Olimpiki duniani kote.
4. Kupitia tamaduni hizi tunajifunza kuwa tunaishi katika dunia iliyo na tamaduni nyingi kama *kuisine*, muziki, dini, na ndoa za kimataifa.
5. Nchi za kimagharibi hasa Marekani zimeonekana kusambaza tamaduni zao duniani kote.

Waandishi wa riwaya teule walichochea kutunga riwaya hizi ili kusawiri mwingiliano wa tamaduni za Kiafrika na tamaduni ngeni hasa za Kimagharibi. Katika sehemu ifuatayo tumejadili mila na tamaduni za Kiafrika kwa kufuata vipengele vifuatavyo:

1. **Malezi ya Watoto**
2. **Mavazi**
3. **Vyakula**
4. **Elimu**

Malezi ya Watoto

Katika riwaya teule kuna ithibati tosha zinazoonyesha kuwa mila na tamaduni zilikuwa zinafuatwa na watu wote. Kwa mfano, katika mila ya Kiafrika mtoto alipozaliwa kitovu chake kilifukiwa katika sehemu fulani. Dhana hii inadhihirika katika riwaya ya *DY*, Bi Mize anapomtokezea Ndi- anamwambia: Nimechomeka chini ya mnazi palipofukiwa kitovu chako. (*DY*, 61)

Kitovu ni sehemu iliyoheshimiwa na Waafrika. Hii ni kwa sababu ilikuwa kama ishara ya uhai. Katika riwaya ya *BA*, mwandishi anatumkumbusha mila na utamaduni wa ulezi wa watoto katika jamii za Kiafrika. Hii inabainika pale Binadamu alipoenda nchi ya Zakongwe:

Tabia hii ilinikumbusha maisha yetu tulipokuwa watoto. Siku hizo tulikuwa tukienda kufuga mifugo ya kijijini pamoja. Hapakuwa na tofauti wala hatukuwazia wapi ni wapi, tuliwalisha pamoja. Tulicheza pamoja. Nakumbuka hata siku hiyo aliyekosa miongoni mwetu aliweza kuadhibiwa na mzazi yeyote sio lazima awe wake. Lakini mambo yalikuwa yamebadilika. (*BA*, 57)

Katika ibara hii inabainika kuwa hapo awali kulikuwa na mila na desturi. Baadhi ya mila hiyo ni watoto kuwa na maadili na heshima kwa watu wazima. Vilevile, tunapata njia ya kuwalea watoto. Ulezi wa watoto ulikuwa wa jamii

nzima. Hakuna mtoto wa mtu. Hii inamaansa kuwa hakuna mtoto angefanya makosa kwa kisingizio kuwa wazazi wake hawamwoni. Mtoto angeadhibiwa na mtu yeyote.

Hata hivyo hali hii ilibadilika kutoka na maajilio ya wakoloni. Kwa mujibu wa Paul na Robin (2007) maajilio ya wakoloni katika bara la Afrika waliathiri mifumo ya kijamii iliyokuweco barani Afrika. Mtagusano huo uliathiri mila na tamaduni na kuvuruga maisha ya wenyeji. Hii inabainika katika riwaya ya *DY*. Yungi anamweleza baba yake:

Lazima [...] uukubali ukweli. Wakati umebadilika. Watoto kuanzia sasa watawaendesha wazee wao. Pia huu ni wakati wa wanawake kuwakimu na kuwaongoza wanaume. [...] Hakuna cha **mila wala desturi**. Hakuna mswalie mtume wala mswalie nini. [...] (M)ajirani wote wanawaachia watoto wao wa kike na wa kiume wafanye wanavyopenda siku hizi [...] Wewe bado unataka kukamata na kudhiti. Unataka uongozi usioweza. Huwezi tena kutuendesha! (*DY*, 25). Msisitizo wangu.

Inabainika kuwa kutokana na maajilio ya wakoloni; mila na tamaduni za Waafrika zimeingiliwa. Hapo awali wazee walikuwa wenye usemi katika jamii, wao ndio walikuwa waelekezi. Lakini imebadilika Yungi anamwambia Ndi-kuwa wao ndio waelekezi. 'Hii si dunia yako Ndi-. Yako imeshapita na umeshaipoteza (*DY*, 209). Aidha, mila na tamaduni za Kiafrika zimempatia majukumu bwana ya kulisha familia yake. Lakini si hivyo katika tamaduni ngeni. Yungi anamwambia Ndi- kuwa wanawake wanaweza kuwakimu wanaume wao. La kushangaza zaidi ni uhuru ambao vijana wanataka katika jamii ya kisasa. Watoto wa kike na wa kiume kufanya yale wayatakayo maishani. Kwa ufupi hakuna mila na desturi katika jamii ya kisasa. Ni kwa sababu ya ukosefu wa mila na desturi katika jamii ya Waafrika ndiyo tulibaini kuwa ndiyo chanzo kuu cha

mivurugo ya jamii ya kisasa. Ndi anasema hivi kuhusu ukosefu wa mila na tamaduni:

Na wao hawalaumiki, ukitazama kasi ya mambo ya usasa na utandawazi inavyosonga. Yetu si yetu tena; ya wenzetu ndiyo tunayoyafanya yetu. Tukitaka tusitake. Mabaya au mazuri! (DY, 26)

Vijana wanafuata mila na tamaduni za kigeni na kuacha yao. Hawataki kusaili iwapo tamaduni hizo ni mbaya au nzuri. Utafiti huu ulibaini kuwa tamaduni hizo za kigeni zimeathiri jamii kwa upande mkubwa sana. Mivurugo ya jamii imesambaa kotekote kutokana na tamaduni ngeni zinazolingizwa katika bara la Afrika hasa kupitia utandawazi:

Na upite muda, si mrefu sana, uje umtazame Yungi. Ni shetani kamili. Anaweza kumbawibu hata walii. Mfuate Bori, utamkuta bweha anayepita kuokota kila uoza na kung'ong'ona kila fupa. Ongozana na Jitu, utamkuta ni pakamwitu, hachelei kuhujumu anapokuwa na haja. Mchungue Dubwa, gombe kasoro mkia! Hana jingine ila wingi wa upumbavu. (DY, 12-13)

Katika dondoo hili, familia yote imesambaratika, kila mtu na dunia yake na mtazamo wa maisha yake. Yungi anashiriki katika ukahaba, matumizi ya dawa za kulevywa na kukosa heshima kwa wazazi wake. Bori alikataa kusoma, Jitu ni mwizi na Dubwa ni mjanja anayelaghai watu.

Fauka ya hayo, uigaji wa tamaduni za kigeni umefanya watu kutoamini rangi ya ngozi yao:

Ah, tunapofika hadi kuona rangi zetu si bora tena, nywele zetu hazifai kamwe, pua zetu, midomo yetu,...midomo yetu...sijui kiasi gani cha ubinadamu wetu kinabaki? Tunabaki tu kuuendeleza ubahashuli wetu kwani kamwe maumbile yetu hayakubali vipodosho na uzuri wa watu wengine. Pamoja na uhodari wetu wote

binadamu, hatuwezi kuukosoa mkono wa Mungu. Hatuwezi kuyakashifu maumbile yetu...nywele fupi, pua, macho, masikio...yote hayo yanahusiana na miili yetu, sura zetu, rangi zetu na hata mazingira...yanawiyana na wapi tunatoka na wapi tupo; na vipendeleo vyetu na nini ulimwengu umetupa na nini umetukosesha: rangi za maumbile yetu, mimea, wanyama na umbile la dunia inayotuzunguka. Tukiiga vyengine ni kichekesho na hatari tu, ingawa hatutaki kuona. (BAF, 51)

Uigaji wa tamaduni zingine imefanya watu kuchukia nafsi zao, maumbile yao na rangi ya ngozi zao. Hii imefanya wao kuanza kutumia vipodozi mbalimbali ili kubadilisha rangi zao. Wengine wameanza kufanyiwa upasuaji ili kubadilisha sehemu za miili yao kama pua, macho na masikio. Wasichana wameonekana wakitumia pesa nyingi kununua nywele zinazouzwa ili kurefusha nywele zao. Hizi zote ni kwa sababu ya kuiga tamaduni zingine zinazotokana na utandawazi. Riwaya ya BA inatuambia tupige darubini mila inayotoka nje:

Tupige darubini hivi vitu tunavyovikimbilia kutoka nje. Hizi video na filamu ni propaganda isiyokuwa ya moja kwa moja. Zinatumiwa kusambaza na kutangaza taswira maalum za utamaduni mmoja tu. Ni ubeberu huu! (BA, 40)

Katika sehemu hii, Binadamu anasema kuwa sio vizuri kuiga tamaduni bila kupiga msasa. Hii ni kwa sababu tamaduni hizi zinaathari hasi katika jamii. Ni njia mojawapo ya nchi zilizoendelea kuendeleza falsafa yao ya maisha na kutunyanyasa kifikra. Vilevile, ubeberu umesababisha maenezi ya tamaduni zisizofaa:

Utamaduni tusioutaka hatuwezi kuuzuia tena. Unakuja kwa mawimbi yenye nguvu. Ngono, ulevi, uchi, matusi, kelele, mavazi ya kuchekesha...Na miili yetu inajazwa sumu. Nyama ya ng'ombe, kuku, kondoo, nafaka,

mbogamboga zinatisha kuliwa. [...]. Kisha ulemavu wa madawa ya kulevyu. (DY, 49)

Tamaduni zisizoendana na mitindo ya kiafrika zimesambazwa kotekote Afrika. Tabia hasi miongoni mwa vijana imejitokeza kutokana na kuiga tamaduni hizi. Vijana wanashiriki katika ukahaba na matumizi ya dawa za kulevyu zinazowalemeza kiakili na kiafya. Ndiposa nchi nyingi barani Afrika zinaugua magonjwa kama saratani.

Mavazi

Katika jamii za Kiafrika mavazi yaliyokuwa yakivaliwa yalikuwa ya heshima. Mavazi ni nguo ambazo huvaliwa na watu ili kufunika mwili au sehemu zake. Mavazi huvaliwa na makusudi mbalimbali: hukinga mwili dhidi ya baridi au jua kali pamoja na athira nyingine za mazingira zinazoweza kuathiri vibaya mwili uchi. Huwasilisha ujumbe kwa watu wengine kwa kuonyesha mtu fulani ni tamaduni gani. Nguo zilizovaliwa na Waafrika zilikuwa na heshima lakini kutokana na maajilio ya wakoloni mitindo ya nguo imebadilika. Kwa mujibu wa Mazrui (1990) mavazi ya Kimagharibi imetamalaki duniani kote. Kila mwanadamu ana mavazi mawili: mavazi ya Kimagharibi na ya utamaduni wake. Ndiposa mtu anayevaa nguo ya Kimagharibi anaona amestaarabika na akivaa nguo ya utamaduni wake anaona yeye ni mshamba. Hii imefanya vijana katika bara la Afrika kubabia nguo za Kimagharibi. Katika dunia ya kisasa, vijana wanavalia jinsi wapendavyo kama inavyojitokeza katika riwaya ya DY:

Mipira miwili kifuani imemsimama, imejaa pumzi tele. Kitopu kimemchupa kidogo juu ya sketi ya mapakupaku ya kitambaa cha setini kilichotemwa mdomoni mwa mbwa. Kitopu kilichoacha mwanya tumboni kwa mshono wa kisasa uitwao 'tumbo-cut'. Sketi yenyewe ilikuwa ya mtindo wa fuNdi-kasahau-mshono'. Miguu chini. Mkono wa kulia sigara inafuka moshi. (DY, 104)

Dondoo hili linatuonyesha jinsi Waafrika hasa vijana wamekengeuka kwa kuvaa nguo za 'tumbo-cut' na fuNdi-kasahau-mshono'. Hizi ni nguo ambazo hazina misingi katika tamaduni za Kiafrika. Nguo hizi zinaacha baadhi ya sehemu za mwili nje. Mara nyingi vijana hawa huwa na utovu wa maadili kama matumizi ya dawa za kulevyu na ukahaba:

Vijana waliokuwemo kundini hapo walicheka na kukariri kila mara yes...yes...huku wakikata miondoko ya ajabu, miondoko ambayo wazee hawajapata kuiona maishani mwao. Miondoko iliyotiwa nakshi na zile suruali walizovaa zilizoitwa mharisho. Ndiyo, wazee wengine waliudhika, lakini hakuna aliyedadisi wala kulaumu chanzo na sababu ya mambo haya ambayo siku hizi yamekuwa mtindo-si ya kupita tu. (DY, 33)

Hapa, mwandishi anatusawiria mitindo mipya ya vijana. Mitindo ya vijana kutembea kundini na kusakata densi za kisasa. Fauka ya hayo vijana hawa wamevaa mavazi yajulikanayo mharisho. Mharisho ni aina ya nguo inayovalikiwa na wanaume. Nguo hii inapovalikiwa huwa inakwamia katika makalio na mtu kuonekana kama anaharisha. Mtindo huu wa mharisho unaleta taswira ya vijana ambao wamekosa adhabu na mara nyingi wazee wanaudhika na aina hii ya mavazi. Inakisiwa kuwa chanzo chake ni uigaji wa tamaduni za kimagharibi zinazosambazwa na utandawazi. Maajabu ni kuwa mtindo huu umekuwa wa kawaida miongoni mwa vijana. Kulingana na riwaya ya BAF, kila binadamu ana haki ya kutenda atakavyo:

Msingi wa haki. Na haki si haki za kawaida tu, bali haki za maraha, haki za watu kufanya wapendavyo...haki ya kuvaa wapendavyo...haki ya mwanamke kuzaa na mume maiti, haki ya kuzalishwa watu kwa sindano...haki na haki na haki... (BAF 44)

Haki za binadamu zimeangaziwa. Haki ya kuvaa. Kila mwanadamu ana haki ya kuhamua aina ya nguo anayopenda kuvaa-fupi au ndefu. Vilevile haki ya kuamua jinsi ya kuzaa imeangaziwa. Iwapo mtu anataka kuzaa kwa njia ya kujamiiana na mume au njia zingine za kibiolojia kama matumizi ya sindano. Utoaji nguo uliendelezwa katika FKK:

FKK ni upeo wa utamaduni. Hivi leo ukitaka kuuangalia upeo wa sanaa tazama mwili wa mwanadamu katika utupu wake. Tazama umbo la mwanadamu katika utupu wake; jinsi Mungu alivyotumba. Ukitaka kuona hivyo nenda FKK... ni kitu kipya FKK, na kipya kina uzuri wake, hasa kibiashara. (BAF, 44)

Katika sehemu hii ya FKK biashara ya utoaji nguo ulifanywa. Biashara hii inatekelezwa hasa na wasichana ambao wanatoa nguo zote na kubakia uchi. Watu hasa wanaume wanapowatazama wanalipia. Sehemu kama hii inapatikana katika riwaya ya *Bina-Adamu*, Binadamu anaonyeshwa na mwelekezi wake hapa:

Palikuwa na watu waliojazana huko. Niliweza kuwaona wazungu wengi na wasichana wengi wadogo ajabu. Baadhi ya wazungu walikuwa wamevua nguo zao. Wasichana wenyewe walikuwa wamevalia vigo vilivyochupa magotini na viblauzi vilivyoachia vitumbo vyao vidogo wazi. (BA, 108)

Tamaduni hizi ya wasichana kutembea uchi kama njia ya kufanya biashara imeenea katika bara la Afrika. Kama inavyodhihirika hapo juu, wazungu ni ishara ya jamii za kimagharibi ambamo tamaduni hii ilipoanzia.

Vyakula

Kwa mujibu wa Rodney (2015) vyakula vya Kiafrika vilikuwa lische bora sana. Rodney anarejelea utafiti uliofanywa na Josue de Castro kabla ya ukoloni na baada ya ukoloni. Utafiti unaonyesha kuwa kabla ya ukoloni afya

ya waafrika ilikuwa bora zaidi lakini ilisoroteka baada ya maajilio ya wakoloni:

1. Katika bara la Afrika halikuwa na magonjwa ya ukosefu wa chakula. Hakuwa na uozo wa meno kutokana na ulaji wa vyakula vya kiafrika. Lakini meno ya waafrika yalianza kuoza baada ya waafrika kukula vyakula vya kigeni.
2. Ujio wa wakoloni ulisababisha ugonjwa wa utapiamlo. Utafiti huu ulifanywa nchini Gambia. Utafiti ulionyesha kuwa baada ya ujio wa wakoloni waafrika walianza kula vyakula bila protini. Wanagambia walikuwa wafugaji wa mifuko na walikuwa wanakula nyama kwa uwingi. Kwa hivyo haingewezeakana wanagambia kuugua utapiamlo.
3. Tafiti katika Afrika ya Kati zinaonyesha kuwa waafrika ambao walikuwa watumwa waliugua magonjwa mbalimbali: beriberi, riketi, na Scurvy. Hii ni kwa sababu watumwa hawa hawangepata vyakula vilivyo na rutubishi.
4. Nchini Afrika Kusini Waafrika walibadilishwa kutoka kula nyama na maziwa hadi kula nafaka pekee. Hali hii ilipelekea waafrika kuugua *pellagra*.

Kutokana na ithibati hizi inabainika kuwa vyakula vya kiafrika vilikuwa vyakula vyenye virutubishi na vya afya. Wakoloni walipofika walitumia propaganda kuwa waafrika hawana lische bora na wanaugua. Hali hii imefanya wahusika kama K katika riwaya ya *BAF*, kubugia vyakula vya wakoloni. Utamaduni wa kigeni unajitokeza kupitia matumizi ya vyakula ambavyo havina asili ya Kiafrika:

Tena mfu akashangaa kuona kijibwa kichanga kilichochoywa na kung'ara dhahabu na kupambwa majani na maua kadha yaliyowiana nacho. Tena akashangazwa na nyama ya nyangumi aliyekaangwa na kukatwa vipandevipande; kombe la *beetles*

waliochemshwa kwa pilipili manga na viungo vyengine na kumwagiwa shonyu na kuzungushiwa jamaa zao mende waliokuwa wakimeremeta wekundu wa kizamoto. Tena makombe ya samaki wabichi, wengine wazima wanapapatikaa, wengine wamekamatwa vipandevipande na katikati limelazwa jichwa lililochomwa ujiti, linapiga makambi mkiani na kutatarisha miba yake; limo ndani ya kigalawa kwa maonyesho ya kupumbaza macho. (BAF, 36)

Hivi sivyo vyakula vya Kiafrika. Mzuka anamwambia K kuwa kama hivi vingekuwa vyakula vya asili ya Kiafrika. Bila shaka ingekuwa na kima na tumbili wa Zaire (BAF, 37). Hii ni thibitisho kuwa vyakula hivi vinavyoliwa katika maeneo ya **Neo-Casino** ni vya kigeni. Vyakula hivi bila shaka vinatokana na tamaduni za kigeni vinavyoingizwa kupitia utandawazi katika bara la Afrika. Madhara yake ni pale K alianza kuugua katika kasri lake:

Alikohoa. Kikohozi yabisi. [...]. Na kisha tumbo likamchiririka kwa sauti ya mnung'uniko. Alilikamata tumbo na kulibinya huku akiguna na kuugua na kukunja uso, na kusikiliza mfereji ukijichia pasi na kizuwizi kutoka pahala fulani tumboni mwake. (BAF, 7)

Vyakula vya kigeni vinamfanya K kuwa na kikohozi kisichoisha. Aidha, tumbo linamwuma na hata kuendesha kwa muda mrefu sana. Hii ni tofauti na vyakula vya Kiafrika K anaandaliwa kijijini mwake na nyanya yake. K anapopelekwa kijijini mwake Kataa anaonekana hataki chakula cha kiafrika:

K aliyekuwa kasita na tonge ya togonya mkononi, alikuwa kayatumbulia macho maduara mawili ya watu waliokuwa wakipambana na chakula utadhani walikuwa na vita nacho [...]. Katika kila kikundi sinia la togonya lilikuwa limetupiwa mboga ya *kikwayakwaya* iliyopikiwa chungu kilicholaziwa vumba la daga. (BAF, 115)

K akiwa kijijini mwake anaandaliwa na nyanya yake Maajuzi vyakula vya asili ya Kiafrika, togonya. K anasema kuwa haziliki. Maajuzi anamwambia kuwa ni chakula chenye asili ya kiafrika na kuwa wao wamekula tangia wadogo na wanaendelea kuwa na afya nzuri. Maajuzi mwenyewe ameishi kwa miaka mingi sana na kuwa na wajukuu. Mjukuu mmojawapo akiwa K.

Elimu

Kwa mujibu wa Rodney (2015) elimu katika mtazamo wa kiafrika ni nguzo muhimu katika jamii na mfumo wa maisha. Elimu inakuwa kutokana na mahitaji ya jamii. Katika jamii za kiafrika nguzo muhimu ya elimu ni manufaa kwa jamii sio mtu binafsi. Baadhi ya sifa za elimu ya bara la Afrika kabla ya maajilio ya wageni ni: uhusiano wa elimu na jamii, elimu ya jamii kwa ujumla, ukuaji wake kutegemea mabadiliko ya jamii, hakuna utengano baina ya elimu na jamii wala kazi za kiakili na kinguvu. Wakati wa maajilio ya wakoloni hali hii ilichukua mwelekeo tofauti. Elimu iliyoletwa na wakoloni inayohimiza ubinafsi, sio elimu inayokuwa katika jamii bali iliyochopekwa, sio ya kuwafundisha watoto lugha na tamaduni zao na itikadi za kiafrika bali kuhimiza itikadi za wakoloni kama ubepari, matumizi ya raslimali asilia. Kwa ujumla elimu ilikuwa ya ukandamizaji, unyonyaji, na uwendazimu. Bara la Afrika likakosa kuendelea na kurudi nyuma kimaendeleo. Haya yanadhihirika katika riwaya ya DY, elimu ilikuwa bure kabla ya ujio wa wakoloni:

Skuli pia niliweza kuendelea, kwani sikulazimika kulipa chochote. [...], elimu ilikuwa bure kwa namna ya bure hasa. Kila mwanafunzi alitolekwa ada kwa mujibu wa mapato ya wazee wake. Mtoto wa kimaskini hohehahe kama mimi sikulipa chochote. Maskini wa kiasi alilipa kwa kiasi chake. (DY 15)

Elimu kabla ya ujio wa wakoloni ilikuwa bure, Ndi- aliweza kusoma bila kulipa chochote. Wazazi wake walikuwa

wamefariki na hivyo alikuwa analelewa na mjomba wake, Omari. Wakati huo elimu ilikuwa na faida katika maisha ya mtu, mwandishi anasema

Wakati ule, si leo, elimu ilikuwa ngazi ya kupanda kwendea maisha ya kipato. Angalau kipato wastani cha kujitosheleza. Mimi, nilipokumbuka nguvu za wazazi wangu na mjomba Omari, nilikuwa tayari kujisabiliana kwa yote kupata elimu. Aaa, leo hata mtoto mchanga anajua kwamba elimu ni upuuzi mtupu. (DY15)

Elimu ilianza kuwa na upuuzi wakati wa maajilio ya wakoloni. Elimu ilirudi nyuma na kukosa kukidhi mahitaji ya binadamu. Haya yanabainika kutokana na mhusika Yungi. Kwa kawaida elimu inafaa kufaidi binadamu. Lakini katika dunia ya leo katika riwaya teule inaonekana siyoy:

Hata ile elimu uliyoisimamia kidete na kunikandamiza nayo kwa maneno na vitendo ili nifaulu katika kila hatua yake, sasa imefaa nini? Hizi ‘A’ nilizonazo katika shahada ya kidato cha sita zinasaidia nini? Mwaka wa saba huu sijapata kazi [...]. (DY 105)

Hapa mhusika Yungi anakashifu mitalaa isiyofaa wanaosomea. Anashangaa hata baada ya kusoma na kupita na alama ya ‘A’ hapati kazi. Maoni kama hayo yanatolewa na Bori anayesema kuwa kufaulu maishani si kupita mitihani tu:

‘sisahau mapenzi yako kwetu. Himiza zako juu ya masomo. Nilikuwa nikichukia kuhimizwa. Kutusimamia kama amirijeshi. Tusome, tusome, tusome. Mimi nilitaka kufanya mengine. [...] Hukunipa nafasi. Na kwa sababu hukunipa nafasi, nilichukia masomo. Ndiyo maana sikufanya vizuri mtihani. Sikulaumu lakini! Nyinyi wazee mmekulia dunia yenu na sisi nyingine. (DY,114)

Bori, anamlaumu babake kwa kuhimiza elimu ya vitabu, elimu ambayo haifai katika dunia yao. Yeye alikuwa na

mawazo tofauti ya kufanya mengine. Hii ilimfanya Bori kuwa mwendawazimu. Upeo wake ni pale Mtima anaposoma na kufaulu shuleni vizuri lakini hakupata kazi. Ilibidi aende ng’ambo ili kutafuta kazi (DY 10).

Elimu ya wakoloni inaenezwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza kama inavyojitokeza katika riwaya ya BAF, Mbomba ambaye ni kiongozi anasema:

Vijana wa siku hizi wasomeshwe Kiingereza bwana. Ili wawe watu wa dunia mpya! Si Kiswahili... Kiswahili ni lugha yao wanayojua, wajifunze nini? Na haitoshi shuleini tu, na nyumbani pia tusiwasemeshe Kiswahili. Nangojea afike miaka minane tu nimpeleke nchi ya jirani, maana sisi hapa hatuna elimu ya maana... walimu hawajui kufundisha Kiingereza. (BAF, 41)

Kiingereza ni lugha ya Kimagharibi iliyoingia barani Afrika wakati wa ukoloni. Inavyoonekana ni kuwa Mbomba anaenzi lugha hii ya kigeni na kudunisha lugha ya Kiswahili. Yeye anaona kuwa Kiswahili ni lugha duni na hata hafai kufundishwa wala kuzungumzwa nyumbani. Mbomba analinganisha Kiingereza na dunia mpya na yuko tayari kuelimisha mtoto wake. Kembo-Sure (2013) anajadili kwa upana matumizi ya Kiingereza barani Afrika. Anasema kuwa maenezi ya lugha ya Kiingereza ni njia mojawapo ya nchi za Kimagharibi kutawala bara la Afrika kiutamaduni, kiuchumi na kijamii; kile Philiposon (1992) anaita ubeberu wa utamaduni na Ngugi (1986) ukoloni wa kiakili. Kemboi-Sure anaona kuwa lugha za kienyeji zinafaa zitumiwe pamoja na Kiingereza ili kustawisha nchi.

Hitimisho

Fasihi yoyote ile haibuniwi kwa ombwe tupu. Fasihi andishi mara nyingi huchota kutoka jamii ambamo fasihi hiyo imeandikiwa. Riwaya teule za utafiti zimerejelea tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kutoka kote duniani ili kuunda ujumbe wao. Imebainika kuwa mivurugo ya jamii

imetokana na jamii ya kisasa kutumia tanzu mbalimbali za fasihi kujifaidi wenyewe. Wanaotaka kuishi kwenye kitovu cha jamii wametumia tanzu za fasihi kuwatisha wengine ili wasifikie kwenye kitovu cha jamii. Fauka ya hayo walio katika pembezoni mwa jamii wanaonelea kuwa ukiushi wa baadhi ya simulizi za jadi ndio chanzo kikuu cha mivurugo ya jamii. Kwa hivyo ili jamii irudi kwenye mahala pake inafaa tujifunze kutoka kwa tanzu za fasihi simulizi.

Dini, Mila na Tamaduni za Waafrika hazijaangaziwa kwa sababa ya kuamini mtazamo wa Kimagharibi. Mtazamo wa Kimagharibi kwa muda mrefu umechukulia Dini, Mila na Tamaduni za Kiafrika kama potoshi, za kimashetani, iliyo giza na chanzo cha kusoroteka kwa uchumi barani Afrika. Utafiti huu umebaini kuwa si hivyo. Zimekuwa propaganda zilizotumiwa na wakoloni ili kuendeleza mizizi yao barani Afrika. Hivyo basi dhana za ubinafsi, ubepari kupenyeshwa katika nchi zetu.

MAREJELEO

- Warnes, C. (2009). *Magical Realism and postcolonial Novel: Between Faith and Irreverence*. New York: Palgrave Macmillan.
- Rodney. W. (2015). *How Europe Underdeveloped Africa*. Nairobi: East Africa Publishers Ltd.
- Rettova, A. (2016). *From Mimesis to Mize: Philosophical Implications of Departures from Literary Realism*. Katika: *Dunia Yao: Utopian/Dystopian in Swahili Fiction*. Cologne: Rudiger Koppe Verlag. C. Vierke, na K. Greven (wah).
- Paul, K. na Robin, C. (2007). *Global Sociology*. Palgrave: Macmillan
- Ndungo, C.M. (1992). *Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Murdock, G.P. (1959). *Africa: Its People and Their Culture History*. Nairobi: Heinemann.
- Mwita-Ssemanda, B. M. (2005). *Dhima ya Ichingero za Wakuria katika Kusawiri Taswira ya Mwanamke*. Chuo Kikuu cha Moi. Tasnifu ya Uzamifu. Haijachapishwa.
- Mbiti, J. (1969). *African Religion and Philosophy*. Nairobi: Heinemann.
- Mazrui, A.A. (1990). *Cultural Forces in World Politics*. London: James Currey.
- Kyamba, A.N. (2018). *Mwingilianomatini Katika Ushairi wa Mnyampala*. Chuo Kikuu cha Moi. Tasnifu ya Uzamifu. (Haijachapishwa).
- Kegley, W.C. na Raymond, G. (2014). *The Global Future: A Brief Introduction to World Politics*. Boston: Wadsworth Cengage learning.
- Kembo-Sure, E. (2013). *Literacy, Language and Liberty: The Cultural Politics of English as Official Language in Africa*. Eldoret: Moi University Press.
- Rettova, A. (2016). *From Mimesis to Mize: Philosophical Implications of Departures from Literary Realism*. Katika: *Dunia Yao: Utopian/Dystopian in Swahili Fiction*. Cologne: Rudiger Koppe Verlag. C. Vierke, na K. Greven (wah).
- Mohamed, S.A. *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mohammed, S.A. *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K.W. (2002). *Bina-Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers.